Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II): Ni kwa Jinsi gani Tutaboresha Utekelezaji katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa?



policy forum

Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II): Ni kwa Jinsi gani Tutaboresha Utekelezaji katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa?

Novemba 2017

Kimeandikwa na: Kikundi Kazi cha Tawala za Mitaa (LGWG) cha Policy Forum

Kimehaririwa na: Daniel Semberya

Michoro na: Simon Regis

Kimesanifiwa na Kupigwa chapa na: Jamana Printers

ISBN: 978 9987 708 29 1

YALIYOMO

MUHTASARI ..... **iv**

SURA 1: UTANGULIZI **1**

Malengo ya FYDP II 1

Vipengele muhimu vya FYDP II 2

SURA 2: UCHAMBUZI NA TATHMINI YA HALI YA UTEKELEZAJI WA FYDP I NA MKUKUTA II **3**

Maendeleo ya Uchumi Mkubwa 3

SURA 3: KUJIPANGA UPYA KIMKAKATI KWA UTEKELEZAJI WA FYDP II **5**

SURA 4: MIRADI / SHUGHULI ZA KIMKAKATI KWA AJILI YA UCHUMI WA VIWANDA NA MAENDELEO YA WATU **7**

SURA 5: MKAKATI WA UPATIKANAJI FEDHA **10**

SURA 6: MKAKATI WA UTEKELEZAJI **12**

(i) Mabadiliko Kuimarisha Shughuli za LED 12

(ii) Mabadiliko Kuhusisha Mahusiano kati ya LGAs na Taasisi za Utafiti na Mafunzo 14

(iii) Mabadiliko Maalum ya – Mamlaka ya Jiji la Dar es Salaam 15

Nafasi na Wajibu wa Mamlaka ya Serikali ya Mitaa 15

SURA 7: UFUATILIAJI NA TATHMINI EVALUATION **16**

Malengo ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E) 16

Mkakati wa M&E Utekelezaji wa FYDP II 17

Majukumu na Wajibu 17

Tathmini ya FYDP II 18

MAPENDEKEZO **19**

MUHTASARI

Mwanzoni mwa mwaka 2016, Serikali ilizindua FYDP II, kwa lengo la kurekebisha mapungufu ya FYDP I na kutoa mpango makini wakati Tanzania inapoanza kuelekea katika maendeleo ya viwanda katika miaka mitano ijayo (2016 – 2021).

Katika kufanya marejeo ya FYDP I, serikali ilitambua kuwa mpango wa awali ulishindwa kufanikisha malengo yake mengi. Wakati Serikali imedhamiria kuwa ukuzaji wa viwanda ni kipaumbele katika miaka mitano ijayo, mapungufu ndani ya mpango unaweza kufanya nchi ishindwe kwa mara nyingine tena kama masuala yaliyojitokeza hayajafanyiwa kazi vya kutosha.

Majadiliano yaliyopita kati ya Serikali na mashirika binafsi yaliyofanyika mwaka 2016, yaliyolenga kufanyia kazi changamoto na masuala ndani ya FYDP II hayajaleta matokeo yaliyokusudiwa. Ili Tanzania ifanikiwe, mbinu mpya na mawazo mapya yanahitajika haraka. Utekelezaji wa ufanisi wa FYDP II utahitaji uelewa wa ndani wa kwa nini majaribio ya nyuma ya kuimarisha viwanda yalishindwa na kuchukua hatua kuhakikisha kwamba makosa ya nyuma hayarudiwi.

Tukitilia maanani juhudi zote ambazo hivi sasa zinafanywa na serikali ya awamu ya tano za kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa nchi ya uchumi wa viwanda ifikapo 2020, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano; Nafasi ya Mamlaka za Serikali ya Mitaa ambayo kauli mbiu yake ni 'Kukuza Viwanda kwa Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu,' unaorodhesha miradi mipya kuwezesha Tanzania kuwa nchi ya viwanda kwa namna itakayoleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii.

Mpango unajumuisha miradi ambayo haijakamilika toka Mpango uliopita na Mkakati kwa pamoja. Pia unatekeleza vipengele vya Dira ya Tanzania ya Maendeleo (TDV) 2025, ambayo ina dhamira ya kugeuza Tanzania kuwa taifa la pato na uchumi wa kati wa viwanda ifikapo 2025. Mpango unatambua kuwa ufanisi wa maendeleo na upunguzaji wa umaskini unahitaji usukumwe na jamii na msaada wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGA).

Pamoja na mambo mengine, Mpango unadhamiria: Kujenga msingi wa kugeuza Tanzania kuwa taifa la uchumi wa kati wa viwanda ifikapo 2025; kukuza maendeleo endelevu ya uwezo wa uzalishaji na uuzaji nje ya nchi, kuimarisha nafasi ya Tanzania kijiografia kwa kuboresha mazingira ya kuendesha biashara na kuiweka nchi kama kitovu cha uzalishaji, biashara na mipango ya usafirishaji kikanda. Kuimarisha upatikanaji wa stadi zinazohitajika viwandani (uzalishaji na usimamizi wa biashara, udhibiti, uhakiki ubora, nk.) na stadi kwa ajili ya shughuli nyingine za uzalishaji na utoaji huduma.

Hivyo, njia ya kuelekea kwenye Tanzania ya viwanda na maendeleo ya watu inafahamika kwa undani na kwamba uhamasishaji wake uko juu katika ajenda ya maendeleo tangu siku za mwanzo wa uhuru. Mbinu zilizotumika, hata hivyo zilikuwa zikibadilika badilika, kwa kutegemea mabadiliko ya kijamii na ya kiuchumi.

SURA 1: UTANGULIZI



Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II) ni zao la muunganiko wa Mpango wa Kwanza wa Miaka Mitano wa Maendeleo (FYDP I) na ***Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania*** - (MKUKUTA II), ambao umejengwa katika nguzo kuu tatu za mageuzi ambazo ni: Uchumi wa viwanda, Maendeleo ya Watu na Ufanisi wa Utekelezaji.

Maudhui ya FYDP II ni: "Kukuza Viwanda kwa Mageuzi ya Kiuchumi na Maendeleo ya Watu" unajumuisha msisitizo wa mifumo miwili, yaani ukuzaji uchumi na mageuzi (FYDP I) na kupunguza umaskini Tanzania (MKUKUTA II). Mpango unaelezea kwa kifupi miradi/ shughuli mpya ya kuiwezesha Tanzania kuwa nchi ya viwanda kwa njia ambayo itageuza uchumi wake na jamii yake.

Pia unajumuisha miradi ambayo haijakamilika kutoka Mpango na Mkakati uliopita. Pia unatekeleza vipengele vya Dira ya Maendeleo ya Tanzania-2025 (TDV) ambayo ina mwelekeo/malengo ya kuigeuza Tanzania kuwa taifa la pato na uchumi wa kati wa viwanda ifikapo 2025.

Malengo ya FYDP II

Mpango huu una malengo yafuatayo:

- Kujenga msingi wa kuigeuza Tanzania kuwa taifa la uchumi wa kati wa viwanda ifikapo 2025.

- Kukuza uwezo wa maendeleo endelevu ya uzalishaji na uuzaji nje ya nchi.
- Kuimarisha nafasi ya ki-mkakati na ya kijiografia ya Tanzania kwa kuboresha mazingira ya biashara na kuiweka nchi kama kitovu cha uzalishaji, biashara na mipango kikanda.
- Kukuza upatikanaji wa stadi za viwandani zinazotakiwa (usimamizi wa uzalishaji na biashara, uendeshaji, uhakiki wa ubora, n.k.) na stadi kwa ajili huduma nyingine za uzalishaji na usambazaji.
- Kuharakisha ukuaji wa uchumi mpana na jumuishi wenye kupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa na kunufaisha watu wengi kwa kuongeza uwezo wa uzalishaji na nafasi za kazi hasa kwa vijana na makundi mengine yanayoishi katika mazingira magumu.
- Kuongeza ubora wa maisha na afya nzuri kwa watu.
- Kukuza na kuimarisha ufanisi wa utekelezaji, vikijumuisha upangaji wa vipaumbele, utaratibu, ujumuishaji na mfungamano wa shughuli/miradi.
- Kuongeza na kuimarisha majukumu ya jamii katika upangaji na utekelezaji, na
- Kuhakikisha kuwa mikataba ya kimataifa na ya kikanda (kwa mfano: Ajenda ya Afrika 2063 na SDGs) inaingizwa kwa kiwango cha kutosha katika mifumo ya upangaji wa mipango ya maendeleo ya taifa kwa manufaa ya nchi.

Vipengele muhimu vya FYDP II

Mpango una vipengele muhimu na vya wazi vifuatavyo:

i. Baadhi ya miradi/shughuli zimewekwa pamoja na kupangwa mkabala na maeneo ya kijiografia au kundi la ushirikiano wa kimaendeleo kuboresha ufanisi wa shughuli za kibiashara ili kuwapatia wawekezaji uchumi-fungamanisho, uratibu na taratibu za kiutekelezaji zikifanyika kimkakati ili kuchochea ushirikiano (utendaji mpana wa miradi/shughuli zenye malengo yanayofanana), ukamilishaji na ufanisi wa hali ya juu.

ii. Mpango unajumuisha kauli mbiu ya "Biashara tofauti", siyo tu kwa ajili ya kukuza ufanisi wa utekelezaji, bali pia kwa ajili ya kukumbatia ubia wa kimkakati na sekta binafsi, kuwezesha maendeleo yake na ushindani na kwa njia ya kuboresha na kuandaa mazingira wezeshi kwa ustawi wake ili yawe endelevu.

iii. Mpango unajumuisha mabadiliko ya kisera na kitaasisi yanayotakiwa ili kuwezesha utekelezaji wake na sekta binafsi ikihamasishwa kuwekeza katika viwanda huku Serikali ikitimiza wajibu wake wa uwezeshaji hasa kwa kuandaa sera wezeshi na mfumo bora wa sheria/kanuni, utengaji wa ardhi, na kuhakikisha miundo mbinu inayohitajika kwa maendeleo ya viwanda ipo mahali pake.

SURA 2: UCHAMBUZI NA TATHMINI YA HALI YA UTEKELEZAJI WA FYDP I NA MKUKUTA II

Sura hii inaelezea kwa kifupi hali ya Tanzania kiuchumi na kijamii. Pia inaonyesha matokeo yanayotokana na tathmini ya utekelezaji wa FYDP I na MKUKUTA II na inatoa uelewa kidogo wa mafanikio na changamoto ili yazingatiwe katika uandaaji wa mpango mkakati wa FYDP II.

Maendeleo ya Uchumi Mkubwa

Mojawapo ya mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa FYDP I na MKUKUTA II, ni ongezeko la wastani wa pato kwa mtu toka Dola za Kimarekani US$ 749.3 (2010) hadi US$ 1,043 (2014). Kadhalika uchumi wa Tanzania umekua kwa kiwango chanya cha wastani wa 7% kwa mwaka.

Moja ya changamoto kubwa ni kwamba sekta ya kilimo imeendelea kuwa nyuma katika kiwango cha ukuaji kwani imekua kwa 3.4% pamoja na ukweli kwamba sekta hii ndiyo inayoajiri idadi kubwa zaidi ya watu (karibu 66.9%).

Changamoto nyingine ni pamoja na ukusanyaji mdogo wa mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs) na utengaji usiokuwa wa hakika wa ruzuku kutoka serikali kuu; utoaji wa fedha usiotosheleza kwa vipaumbele katika uwekezaji na ushiriki mdogo wa sekta binafsi. Hali hii inahitaji ufanisi katika uimarishaji wa usimamizi wa fedha za umma katika mabadiliko (reforms) yanayoendelea.

Changamoto nyingine za kijamii na za kiuchumi zilizotajwa ni tofauti kubwa zinazoendelea kuwepo kati ya maeneo ya mijini na vijijini, kuhusiana na upatikanaji wa maji safi na salama na miundo mbinu ya usafi na huduma. Kuna ongezeko la tofauti katika usawa kati ya mikoa tajiri na maskini katika huduma zinazotolewa na LGAs. Utengaji usiotosheleza wa fedha na rasilimali watu unaendelea kuwa changamoto kubwa inayozuia mafanikio zaidi katika upatikanaji wa maji safi na salama, pia huduma bora za afya na elimu.

Kwa upande wa utawala bora na uwajibikaji, mpango unaeleza kwa kifupi uboreshaji kama vile kubadilisha mfumo wa usimamizi wa fedha za umma (ukaguzi wa ndani na nje), kuboresha mifumo ya usambazaji huduma (afya na elimu), kuimarisha maendeleo ya kitaasisi (watunga kanuni, sera na sheria), kuboresha uwajibikaji, uwezo wa LGAs kuwa huru katika kujiamulia vipaumbele vyao vya maendeleo, na katika kukuza na kusimamia rasilimali zao.

Hata hivyo uwepo wa rushwa kubwa na ndogo, udhaifu katika uwajibikaji unaosababisha utoaji duni wa huduma za jamii, mifumo ya umma iliyo dhaifu zimebaki kuwa changamoto.

Zaidi ya hayo, mpango unadhamira ya kujenga uwezo wa jamii kupitia ugatuzi wa madaraka kama unavyosema katika ujumbe wake muhimu namba nne ya kwamba, ugatuzi wa madaraka haujajenga uwezo wa jamii kikamilifu, kwa hiyo katika mpango huu serikali itajizatiti kuhakikisha ukuaji mpana na maendeleo yanapatikana kupitia ugatuzi wa madaraka katika misingi ya jamii kujisaidia na Serikali kuwezesha pale inapokwama pia inayowapa uwezo jamii na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs) kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo yao kwa mbinu ambazo ni endelevu kwa maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi ambayo ni jumuishi.

SURA 3: KUJIPANGA UPYA KIMKAKATI KWA UTEKELEZAJI WA FYDP II



Mageuzi ya muundo na maendeleo ya watu yana umuhimu mkubwa sana Tanzania kwani yanachangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi, hasa Pato la Taifa (GDP). Kihistoria Tanzania ilipata uzoefu wa mabadiliko makubwa katika jaribio lake la awali la mageuzi ya kimuundo na maendeleo ya jamii (yaani uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu) tangu miaka ya 1960.

Sura hii inaeleza upangaji upya wa kimkakati kwa utekelezaji wa FYDP II ili kukuza viwanda kwa ajili ya mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu Tanzania.

Pia inaonyesha mambo muhimu yaliyoainishwa na tuliyojifunza ambayo yatasaidia katika uchaguzi wa mbinu ya kupanga upya mfumo wa utekelezaji unaoendana na mwelekeo wa FYDP II (kama unavyoelezwa katika sura ya 4).

Mwelekeo wa Tanzania ya viwanda na maendeleo ya watu umeelezwa kinaganaga na utangazaji wake ni mkubwa katika ajenda ya maendeleo tangu siku za mwanzo za uhuru. Hii mbinu hata hivyo haijawa thabiti, ikiyumbishwa na mabadiliko katika hali ya kijamii na kiuchumi nchini.

Mwanzoni mwa miaka ya 1960, nchi nyingi za kiafrika ziliamua kuchagua maendeleo ya haraka na ukuaji wake kijamii na kiuchumi, ambapo mwanzoni utekelezaji ulienda vizuri, hususan Tanzania kuanzia kipindi cha uhuru hadi Azimio la Arusha ilikuwa na viwanda vilivyoanzishwa vipatavyo 186 ikiwa ni pamoja na

ujenzi, umeme, gesi, uchimbaji madini na uchimbaji kokoto katika mikoa mbali mbali ambavyo viliajiri idadi kubwa ya watu na vilichangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi vikitoa ajira zipatazo 200,000 na kuchangia asilimia 4.3 katika pato la Taifa (GDP) na kuongeza kiwango cha biashara kwa kiasi kikubwa.

Kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) mwaka 1964 pia kulichangia kwa kiwango kikubwa katika mafanikio haya ya ukusanyaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya viwanda na hivyo kuleta fursa za ajira na kuongeza kipato.

Kwa bahati mbaya, hizi harakati nzuri zilikandamizwa na mazingira ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ulimwenguni na hivyo kati ya mwaka 1975 hadi 1981 ukuaji ulikuwa 0.6%, ulishuka hadi kufikia namba hasi ya -3.9% kati ya mwaka 1981 hadi 1985.

Katika miaka ya 1980 hadi 1990, Serikali ilijaribu mipango mbali mbali kama vile: Mipango ya kurekebisha muundo (SAPs) na mpango wa kufufua uchumi (ERP) ambayo ilikuwa na masharti magumu ili kuondokana na hiyo hali tete ya kiuchumi. Kutokana na masuala yaliyojitokeza na ambayo yalitetewa na SAPs pamoja na wafadhili wa nchi za magharibi, na changamoto walizozileta, Tanzania inahitaji kuwa na msingi imara wa viwanda na mikakati itakayotuinua kutoka hali hii na kufikia mwisho tunao utarajia yaani 'Tanzania ya Viwanda" kama anavyosisitiza Mheshimiwa Raisi John Pombe Magufuli.

Zaidi ya hayo, ili kuweza kufikia hatua ya kuwa nchi ya viwanda kunahitaji taasisi zenye nguvu na zilizodhamiria, ambazo ni pamoja na mashirika yanayohusika na upangaji bei na masoko, makampuni na viwanda, taasisi za fedha, utawala bora na Serikali kutekeleza wajibu wao katika kuleta maendeleo.

Ili Tanzania iwe nchi ya kipato cha kati (uchumi wa viwanda), Serikali kuu inabidi ishirikiane na Serikali za Mitaa ili kufuatilia uwekezaji. Mfungamano wa sera za taifa yaani: Biashara, viwanda, kilimo, elimu na maji, umeme, ajira n.k. ni muhimu pia.

SURA 4: MIRADI / SHUGHULI ZA KIMKAKATI KWA AJILI YA UCHUMI WA VIWANDA NA MAENDELEO YA WATU

Sura hii inatambua hitaji la kukusanya watu wakubali kuwa nyuma ya utekelezaji wa huu mpango ili kuvutia ushiriki wa wananchi kutoka ngazi zote. Hili hatimaye litawezesha kufikia malengo ya mpango na matarajio yaliyopangwa katika Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025.

Mpango unataja ujumbe muhimu katika maeneo 10 kama mafunzo yanayotokana na utekelezaji wa mpango uliopita yaani FYDP I na MKUKUTA II ili yazingatiwe kwa utekelezaji wa ufanisi wa mpango wa awamu hii.

Kwa ajili ya utawala wa serikali za mitaa unataja ujumbe namba nne ambao ni: ‘‘Zoezi la Madaraka kwa Umma na Maendeleo ya Jamii Kiuchumi halijajenga uwezo wa jamii kwa kiwango cha kutosha.” Ni wazi kwamba Usambazi wa huduma wenye ufanisi unahitaji mifumo ya ugatuzi wa madaraka inayokidhi mahitaji ya jamii kwa wakati unaotakiwa.

Hali kadhalika, ugatuzi wa madaraka ni muhimu katika kuhakikisha kuwa ukuaji (kiuchumi) ni mpana na unajumuisha jamii zote na sehemu kubwa ya watu nchini (ikiwa ni pamoja na wakulima wadogo wadogo na wafanya biashara wadogo).

Mpango huu wa kimkakati unajumuisha tofauti za maeneo (spatial) katika maendeleo kupitia ugatuzi wa madaraka kwa kutegemea kanuni ya kusaidiana (subsidiarity), inayojenga uwezo wa jamii na mamlaka

ya serikali za mitaa (LGAs) kutumia kwa njia endelevu rasilimali zilizopo katika maeneo yao kwa ajili ya maendeleo jumuishi yatakayonufaisha wote kijamii na kiuchumi.

Wakati ufafanuzi mpana wa neno viwanda unajumuisha shughuli kama vile uchimbaji madini na kokoto, utengenezaji bidhaa viwandani, umeme, gesi, usambazaji wa viyoyozi / vifaa vya kurekebisha hali ya hewa, usambazaji wa maji, ukusanyaji wa majitaka, uzoaji wa taka ngumu na shughuli za marekebisho na ujenzi, utengenezaji bidhaa viwandani umeainishwa chini ya huu mpango kuwa ndiyo unaoongoza katika mchakato wa kuelekea kwenye uchumi wa viwanda.

Kwa kupitia mpango huu Tanzania inazingatia huu ukweli kwa sababu za kitaifa na kimataifa kama vile: Kihistoria sekta hii (ya viwanda) imekuwa muhimu katika kusukuma maendeleo ya kiuchumi; sekta hii imekuwa eneo lenye ujuzi mkubwa kwa uchumi na lenye kupokea maendeleo ya teknolojia; ina uwezo mkubwa zaidi kiuzalishaji na uwezekano wa ubunifu; na ya kwamba ushindani wa uzalishaji viwandani ni mojawapo ya vitambulishi vya ukuaji endelevu kwa muda mrefu.

Ili kufikia malengo yaliyopangwa kwa sekta ndogo ya uzalishaji viwandani, Mpango utatekeleza shughuli/miradi ifuatayo;

Kuunda mazingira wezeshi na mfumo madhubuti kuwezesha uzalishaji viwandani; hii itajumuisha uanzishaji wa kanda maalum za uchumi na mauzo nje ya nchi, kituo cha utaratibu wa ugavi na usafirishaji wa watu na vitu, maeneo ya viwanda, (industrial parks), taasisi za utafiti na maendeleo; na kukuza biashara ndogo ndogo na za kati kwa kuzingatia yaliyomo katika jamii.

Mpango unatarajia kuendeleza / kukuza uwezo wa uzalishaji katika mafuta ya viwandani (petroli) na bidhaa zake, jengo la bohari ya madawa na ujenzi wake, usindikaji wa bidhaa za kilimo, makaa ya mawe, chuma na chuma cha pua.

Katika hili ni muhimu kuzingatia shughuli/miradi ya aina nne kuhusiana na uchimbaji madini na vyuma. Hii ni pamoja na:

- Unufaikaji kutokana na madini.
- Ubia wa masharti (kat ya wageni toka nje-wananchi, mkubwa-mdogo).
- Uwepo wa miundombinu hasa reli, barabara na nishati.
- Mafunzo na uendelezaji wa stadi.

Kwa upande wa biashara ya ujenzi ambayo ni moja ya shughuli muhimu za uchumi nchini Tanzania; sekta hii imetawaliwa na makandarasi wa kigeni ambao wanapata zaidi ya 60% ya thamani ingawaje hawafikii hata 10% ya makandarasi waliosajiliwa hapa nchini. Ilikuweka uwiano sawa, Mpango, unaweka nguvu zaidi katika kuhamasisha na kuimarisha makampuni ya ndani kushiriki kwa ufanisi katika sekta ya ujenzi ili kuwawezesha kupata mgawo wa haki katika ukuwaji mkubwa wa sekta ya ujenzi unaotarajiwa.

Mpango huu unaelezea kilimo kuwa ni msingi kwa ukuaji wa uchumi wa viwanda Tanzania, na kinategemewa kuchangia jumla ya ajira zote kwa 56.5% ifikapo mwaka 2020 kukiwa na mikakati ifuatayo:

- Kurefusha na kupanua mnyororo wa thamani kwa kukuza stadi.
- Kukuza ubunifu katika utafiti na maendeleo.
- Kuboresha miundombinu.
- Kukuza vikundi vya uzalishaji, biashara ndogo na za kati.
- Masoko mbadala ya bidhaa na ufikiaji wa huduma za fedha.

Mpango umetoa vipaumbele kwa mazao yafuatayo katika kilimo: a). Kwa mazao - mahindi, mpunga (mchele), alizeti, jamii ya kunde na maharage, kilimo cha maua, pamba, katani, zabibu, ufuta. b). Kwa mifugo – nyama ya ngombe, ngombe wa maziwa, kuku, ngozi iliyosindikwa na ngozi ya kawaida c). Kwa uvuvi na mazao ya majini – uvuvi wa samaki katika maji ya kawaida (mito na maziwa), uvuvi wa kando

kando ya bahari na ndani kabisa ya bahari pamoja na ufugaji wa samaki katika mabwawa/madimbwi yaliyojengwa kwa ajili hiyo.

Kuhusu usimamizi wa rasilimali za asili, mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa Mpango unaweka msisitizo katika kulinda wanyama pori na kutumia mbinu shirikishi za kuwezesha jamii kubadili taratibu fulani za maisha yao ili kuhimili mabadiliko ya hali ya hewa pamoja na kuagiza miradi mikubwa kufuata utaratibu uliokubalika wa tathmini ya matokeo kwa mazingira na kanuni za ukaguzi. Miradi/shughuli zinazohusika na haya yanayosisitizwa ni pamoja na uhifadhi wa maliasili, kuimarisha mfumo wa usimamizi wa maliasili kwa ngazi za jamii, na ukuzaji wa teknolojia ya nishati jadidifu (renewable green energy).

Kuhusu ukuaji na uchumi wa viwanda, Mpango umetambua utalii na hitaji la kuufanya uwe wa ndani, pia kuandaa mazingira wezeshi kwa sekta ili kuongeza utangazaji wa Tanzania kama sehemu yenye uzuri wa pekee kwa utalii. Sekta hii inategemewa kuchangia katika jumla ya ajira kwa kiwango cha 12% ifikapo mwaka 2020. Ili utalii uweze kustawi Tanzania, Mpango umeweka juhudi za kuboresha miundombinu ya kuvutia watalii, kufunza watu wake kutimiza wajibu na kufikia viwango vinavyotakiwa katika biashara hiyo.

Zaidi ya hayo, Mpango unasisitiza maendeleo ya watu kama jambo la msingi kwa mafanikio ya ukuaji na uchumi wa viwanda. Pia inatarajia kukuza elimu, stadi zinazofaa na kuboresha hali ya afya ya kila mmoja na jamii kwa jumla. Ni chini ya huu mkakati kwamba huduma za jamii hasa katika ngazi ya serikali za mitaa (jamii) zitatekelezwa kwa ufanisi. Katika elimu kwa mfano; uwiano wa mwalimu-mwanafunzi kwa ngazi zote, mazingira ya kufundisha na kujifunza yataboreshwa, na wanafunzi walioko katika ngazi ya elimu ya juu watawezeza kupata mikopo, matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika kufundisha na kujifunza yatapanuliwa na mishahara pamoja na nyumba za waalimu zitaboreshwa.

Mpango pia unayo shughuli/miradi ya afya kama vile kuimarisha mifumo ya afya ya msingi na rufaa, kupatia mahospitali vifaa vya kisasa na kutoa mafunzo kwa watumishi wa afya na tiba kwa magonjwa yasiyoambukiza, kuboresha mishahara na nyumba za watumishi wa afya pamoja na msisistizo maalum katika madawa ya kinga na udhibiti bora wa magonjwa ya mlipuko. Haya yakifanyika idadi ya vifo vya watoto wa chini ya umri wa miaka mitano na vya wakina mama vitapungua kwa kiasi kikubwa, umri wa kuishi utaongezeka hadi miaka 66 na kuendelea kwa VVU/UKIMWI kutapungua na kuwa 3% tu.

Ili kuwezesha yaliyotajwa hapo juu, Mpango una taratibu zilizopangwa kwa ajili upatikanaji wa maji na uboreshaji wa usafi kwani utahifadhi rasilimali maji na vyanzo vyake, utajenga miundombinu ya kuvuna maji na maabara za maji, ujenzi wa mitambo ya kudhibiti majitaka, mitambo ya kuhifadhi, mabwawa ya kutibu maji, mabomba ya kupitisha maji taka, kukarabati miundombinu ya maji masafi na maji taka, pia kujenga stadi na uwezo wa watumishi wa ngazi zote zinazotakiwa (uvunaji, upitishaji, usambazaji na utoaji hati za madai).

Mpango una shughuli/miradi kadhaa ya kimkakati kwa ajili ya kulinda makundi yaliyoko kwenye mazingira magumu na kuhakikisha uwepo usalama wa chakula kwa ajili ya wananchi wa vijijini na wa mijini. Pia unafuata misingi ya utawala bora ambayo ni pamoja na utawala wa sheria, demokrasia, na vipengele vingine vyote vya utawala bora kama vile ufanisi, uwajibikaji, uwaminifu, uwazi, (yaani: LGAs zote ziweke wazi bajeti zao, mapato na matumizi halisi katika mbao za matangazo ili zifikiwe na kusomwa na umma kwa urahisi) ushiriki na ulinzi wa haki za binadamu kwa wote hasa kwa makundi yaliyoko katika mazingira magumu.

Mpango pia unasisitiza usalama wa taifa na wa mtu binafsi na mali, kukuza na kuendeleza utamaduni wa uzalendo na bidii ya kazi, uadilifu na moyo wa kujiamini, wakati huo huo kuboresha huduma kwa umma, na wote kupata haki ni mambo ya msingi kwa dhamira ya Mpango.

Kwa hiyo, sura hii inaonyesha njia wazi ya mazingira wezeshi kwa uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu kwa kuendeleza uimara wa uchumi, kuboresha miundombinu na uwezekano wa urahisi wa kuendesha biashara pamoja na kuweka juhudi za ziada katika “miradi ya kielelezo” (flagship projects) yaani, miradi “itakayoweza kuchochea mabadiliko tunayowania ya Tanzania ya uchumi wa viwanda na mageuzi ya kijamii na kiuchumi” kwa nchi nzima.

SURA 5: MKAKATI WA UPATIKANAJI FEDHA

Sura hii inapendekeza hatua za kukamilisha utekelezaji wa bajeti kwa ufanisi na kukuza ubashiri wa rasilimali fedha ili kuimarisha utimizaji wa wajibu na ahadi za serikali za kutuma fedha kwa ajili ya Mpango. Mafanikio katika utekelezaji wa Mpango kunategemea, pamoja na mambo mengine, katika uwezo wa taifa kukusanya rasilimali fedha, kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi pia uwezo wa kutumia rasilimali hizo kwa ufanisi.

Inakadiriwa kuwa jumla ya shilingi za Tanzania trilioni 107 zinahitajika kwa utekelezaji wa Mpango. Fedha hizi zitakusanywa kutoka serikalini, sekta binafsi na wabia wa maendeleo. Serikali inategemea kuchangia karibu shilingi za Tanzania trilioni 59 au wastani wa shilingi za Tanzania trilioni 11.8 kwa mwaka kwa kipindi cha Mpango. Zilizobaki zitaombwa kutoka sekta binafsi na wabia wa maendeleo.

Serikali imepanga kutumia kati ya 30% hadi 40% ya bajeti ya serikali ya maendeleo, kwa kuanzia na shilingi za Tanzania trilioni 11.8 kwa mwaka wa fedha 2016/17, kwa matarajio kwamba hiki kiwango kitapanda hadi kufikia shilingi trilioni 13.5 kwa mwaka wa fedha 2020/21, kama ukusanyaji wa rasilimali ukiboreshwa.

Ili kufikia malengo haya, mabadiliko kabambe yamepangwa kuwezesha ongezeko katika ukusanyaji wa rasilimali za ndani kutoka vyanzo vya sasa pia kwa kupanua wigo wa kodi. Uhamasishaji wa fursa za uwekezaji/biashara umesisitizwa kwa mtazamo wa kuboresha utambuzi na uandaaji wa miradi ili kuvutia mitaji binafsi, kwa njia zote mbili yaani, ushiriki binafsi na na kwa ubia.

Hivyo, Mpango unaanza kutumia sera mpya ya fedha na mikakati mipya ili:

i. Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani;

ii. kuongeza ushiriki wa sekta binafsi, kwa taasisi moja moja au kwa ubia na sekta ya umma;

iii. kuhakikisha kuwa uwekezaji wa kipaumbele unapata fedha kikamilifu bila vikwazo vyovyote ili kupata matokeo tarajiwa;

iv. kuendeleza soko la ndani la fedha na hasa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya maendeleo ya muda mrefu kwa ushirika wa mashirika yenye malengo yanayofanana na utoaji wa fedha kwa pamoja; kutumia nguvu ya ushawishi wa rasilimali za sekta ya umma;

v. kuvutia ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya vipaumbele; na

vi. kujenga usimamizi mzuri wa madeni.

Kwa mujibu wa Mpango huu, serikali itawezesha Mamlaka ya Serikali za Mitaa kupanga njia na taratibu za kuinua kodi ya majengo kama chanzo muhimu cha mapato kwa kuanzisha taratibu thabiti za uthaminishaji ili kupanga viwango vinavyofaa na kuvipitia mara kwa mara; kuanzisha mahusiano ya ki-utendaji katika usimamizi wa kodi ya majengo na kuhamasisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs) kuchukulia kodi ya majengo kama chanzo muhimu cha mapato.

Serikali itapitia mifumo iliyopo ya kubakiza wafanyakazi kazini kwa muda mrefu kwa mtazamo wa kuwamotisha kwa ajili ya wafanyakzai wa wizara, idara na wakala wa serikali (MDAs) kufuatilia kwa bidii ukuaji endelevu katika mapato yasiyolipiwa kodi (NTR). Zaidi ya hayo, serikali itaanzisha mifumo inayofaa itakayo hamasisha (itakayomotisha) LGAs kufuatilia ukusanyaji wa mapato kama kiashiria muhimu cha utendaji, kwa afisa mmoja mmoja na kwa idara husika.

SURA 6: MKAKATI WA UTEKELEZAJI

Kuhakikisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa inashiriki kikamilifu katika muundo wa utekelezaji, Mpango umeainisha yafuatayo:

Kuimarisha Ushiriki wa Jamii Kupitia Mbinu ya Kuendeleza Jamii Kiuchumi (LED)

Ili kuhakikisha matokeo yanayotokana na ukuaji uchumi pamoja na utoaji huduma yanatiririka hadi katika ngazi ya jamii na kaya, Mpango unafadhili ugatuzi zaidi wa madaraka ya serikali kuu ili kuweza kukidhi mahitaji ya jamii kwa muda muafaka. Mamlaka ya Serikali za Mitaa lazima zizidi kujengewa uwezo ziweze kufanya maamuzi ya mipango inayorandana na vipaumbele vya Mpango. Huku kufanya Mpango kuwa wa kijamii zaidi kutatoa njia ya kuzifanya SDGs kukubalika na jamii na hivyo jamii kuziona ni zao. Hii itahusisha kuhamisha madaraka na rasilimali kwenye ngazi ya jamii kama ifuatavyo:

(i) Mabadiliko Kuimarisha Shughuli za LED

Mabadiliko yafanyike ili kuimarisha mageuzi kutokana na ugatuzi mkubwa zaidi wa madaraka, uwajibikaji na uwazi. Hii ifanyike sambamba na kuingiza mbinu za "Matokeo Makubwa Sasa" (BRN) katika ngazi ya jamii. Pamoja na hayo, juhudi zielekezwe katika kuhakikisha kuna uratibu wa ufanisi kati ya watendaji wa MDAs, RSs, na LGAs ili kuandaa mazingira mazuri kibiashara kwa sekta binafsi kushamiri. Hili pia

litahusisha utekelezaji wa kazi ambayo haijakamilika ya Mpango wa Mabadiliko ya Serikali za Mitaa (LGRP) inayojumuisha utawala (usimamizi wa rasilimali watu) na ugatuzi wa madaraka ya fedha; pamoja na ulinganifu wa sheria katika ngazi ndogo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LLGA).

Wajibu wa LGAs kuhusu mbinu hii ni wa muhimu sana kwa masuala yanayohusu utoaji / utengaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji, uendelezaji wa vikundi vya biashara ndogo na, msaada kwa shughuli/miradi ya LED nk. Lengo kuu la LED katika Mpango ni kuhakikisha kwamba mbinu za kivitendo zinatumiwa na RSs, LGAs, na Jamii katika kuandaa na kutekeleza shughuli zinazohusu jamii. Upangaji wa ufanisi wa LED unahakikisha kuwa masuala ya kipaumbele yanafanyiwa kazi na rasilimali kidogo iliyopo inatumika vizuri kuchochea ukuaji na upunguzaji wa umaskini.
Ili ukuaji na matokeo ya miradi/shughuli nyingine ziwafikie na kuwanufaisha jamii iliyoko katika ngazi ya chini kabisa, Mpango unahitaji uendane na hali ya jamii, jambo ambalo linahitaji uwezo mkubwa kiutendaji katika ngazi ya jamii. Kwa kutambua uwezo mdogo wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs), Mpango unapendekeza kuwa uwezo ujengwe na kuimarishwa kufuatana na mikakati muhimu ya LED kama ifuatavyo:

- Taratibu za utoaji zabuni na manunuzi za Mikoa na LGAs zitayarishwe kwa jinsi ambavyo makandarasi wadogo na wafanya biashara ndogo ndogo wanaweza kushinda na hivyo kunufaika.

- Kuzitafutia soko fursa za uwekezaji kwa wafanya biashara wa ndani na nje ya nchi, pamoja na kufadhili vituo vya huduma vinavyotoa msaada na taarifa kwa wafanya biashara wanaotaka kuanzisha biashara katika maeneo yao ya mamlaka;

- Kujenga ushirikiano/muungano ndani ya jamii, kwa kusudi la kujenga taasisi ndani ya LGAs na kutumia rasilimali za sekta binafsi zinazoweza kuleta na kuwezesha mabadiliko ya sera kwa maendeleo ya sekta binafsi;

- Kufadhili kinachoitwa "Maktaba Hai" ambavyo ni vituo vya maonesho yanayolenga katika kuonesha kwa vitendo ni kitu gani kinafaa katika maeneo husika na kutengeneza ajira endelevu na manufaa halisi kwa jamii;

- Kuwezesha jamii kutatua matatizo yao ya kiuchumi wenyewe, ikiwa ni pamoja na kubuni na kujaribu mawazo mapya ya kuboresha upatikanaji kazi kwa ajili ya makundi yanayoishi katika mazingira magumu na walio wachache;

- Kuhakikisha kuwa mazingira ya ndani ya uwekezaji yanafaa kwa kusaidia biashara ndogo ndogo za ndani SMEs na kuvutia biashara mpya pamoja na kuvutia uwekezaji wa ndani;

- Kuwekeza katika miundombinu (migumu) kwa kuboresha barabara, mifumo ya majitaka, viwanja vya ndege, n.k. kwa ajili ya biashara; Kuwekeza katika miundombinu laini ikiwa ni pamoja na kuendeleza rasilimali watu, kufadhili taasisi na masuala ya kanuni na sheria;

- Kuwezesha ukuaji wa vikundi vya biashara ambavyo viko eneo maalum la kijiografia kwa ajili ya kufufua ukuaji (yaani maeneo fulani ya kijiografia ikiwa ni pamoja na vikundi vya jamii vinavyoishi katika mazingira magumu);

- Kuwezesha vyama vya ushirika vya msingi vyenye shughuli maalum, kutumika kukusanya mazao/ bidhaa kutoka kwa wakulima wadogo wadogo au viwanda vidogo na vya kati vya uzalishaji bidhaa au kusaidia katika manunuzi ya pamoja kama njia ya kuhakikisha mahusiano ya nyuma na mbele ambayo matokeo yake ni mtiririko kidogo kidogo wa manufaa na upunguzaji wa umaskini,

Kwa nyongeza, Mpango unatambua kwamba maendeleo ya ufanisi na upunguzaji wa umaskini unahitaji uongozwe na jamii yenyewe kwa msaada wa LGA. Jamii huanza mchakato wa upangaji wa mkakati wa LED kwa kuainisha watu, taasisi za umma, biashara zilizopo, mashirika/asasi za kiraia, na makundi mengine yenye maslahi (wadau) katika uchumi wa jamii.

Stadi na rasilimali ambazo kila mmoja wa hawa wadau analeta katika mchakato wa upangaji mkakati

ni muhimu sana kwa msingi wa mafanikio. LGAs na RAs watakuwa na wajibu wa kuhakikisha mazingira ya biashara yanafaa hasa kwa biashara ndogo ndogo na za kati (MSMEs). Mafanikio/maendeleo katika kipengele hiki yata tathminiwa kupitia utafiti wa mazingira wezeshi kwa biashara (BEE). Serikali itawezesha utatuzi wa changamoto zitakazotokana na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya LED, kwa kuwa LGAs nyingi huwa hazina rasilimali za kutosha kufanikisha LED.

Kupitia Mpango huu, Serikali itaongeza utengaji wa rasilimali kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Hii itahitaji utayarishaji wa fomula inayofaa kwa ajili ya ruzuku ya LGAs kutoka Serikali Kuu na kuweka taratibu za kulinda matumizi ya LED zisitumike kwa matumizi mengine, ili kuhakikisha kuwa LED inakuwa chombo cha kuleta mabadiliko katika jamii.

Vyanzo vya fedha za shughuli za LED ni pamoja na:

(a) Mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yanayotoka katika vyanzo vyake vya siku zote, tahadhari ikichukuliwa kujikinga na mtego wa kuanzisha kodi zenye usumbufu.

(b) Ugatuzi wa fedha kutoka Serikali Kuu, kwa mfano shilingi za Tanzania milioni 50 kwa kila kijiji.

(c) Ruzuku toka kwa wafadhili – pamoja na Asasi za kimataifa zisizo za serikali, Mifuko ya fedha za misaada k.m. zile zinazohusika na hifadhi ya mazingira.

(d) Fedha toka sekta binafsi kama vile fedha kutokana na wajibu wa makampuni makubwa kwa jamii.

(e) Mifuko ya fedha za misaada, hasa kwa uhifadhi wa mazingira na uboreshaji, shughuli zinazohusu rasilimali watu, na upunguzaji wa umaskini.

(f) Pale inapowezekana, LGAs na watendaji wengine katika ngazi ya jamii watahamasishwa kuanzisha shughuli zao binafsi za kuwawezesha kupata rasimali fedha zaidi ya ruzuku toka serikali kuu.

(g) Kuanzisha Mashirika/Makampuni ya Maendeleo ya Mkoa kama chombo cha kisheria zikiwa na shughuli zinazofanana na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) ili kukusanya fedha kwa ajili ya miradi katika maeneo yaliyo chini ya mamlaka yao.

Ili kuhakikisha ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za LED, LGAs zitawezeshwa kufanya utafiti wa BEE ili kupata taarifa ya maoni ya wananchi ya hali na kanuni zinazowaathiri wao na biashara zao, kwa lengo la kujulisha sera na taratibu zinazozuia maendeleo ya biashara; vile vile, kuainisha masuala muhimu yanayohusu eneo lao.

Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Ofisi ya Raisi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaandaa mwongozo wa kuanza utekelezaji wa mbinu ya LED. Mwongozo utajumuisha, pamoja na mambo mengine mbinu za kupima utendaji wa shughuli zinazotekelezwa katika ngazi za Mikoa na LGAs, kusudi wananchi waweze kuelewa hali ya maendeleo yao. BEE kitakuwa chombo kimojawapo cha kutathmini utekelezaji kwa ngazi ya jamii.

Utendaji wa ufanisi wa LED kwa ujumla, utaongeza wigo wa masuala ya uchumi na vyanzo vya mapato vya Serikali husika na hivyo basi, hatua kwa hatua, kutapunguza utegemezi mkubwa kwa Serikali Kuu. Ongezeko katika hatua za maendeleo ndani ya jamii kutapunguza mwenendo wa uhamiaji wa watu kutoka vijijini kwenda mijini na hivyo kupunguza mzigo wa utoaji wa mahitaji ya kijamii mijini na miundombinu.

(ii) Mabadiliko Kuhusisha Mahusiano kati ya LGAs na Taasisi za Utafiti na Mafunzo

Kujenga uwezo wa LGAs (pamoja na LLG) kusimamia, Serikali itafadhili mafunzo kazini(internships) na shughuli za kujitolea kwa wanachuo waliofuzu vyuo vikuu waliopitia mafunzo yanayohusu maendeleo ya vijiji na/au Serikali za Mitaa yanayotolewa na vyuo kama vile Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo; Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Chuo cha Mifugo (LITI) na Chuo cha Kilimo (MATI). Hata pale watakapokuwa wakijenga uwezo wa LGAs na LLGs, huu utaratibu pia utawapa washiriki fursa ya kujifunza changamoto halisi za maendeleo vijijini na jinsi ya kuzitatua, jambo ambalo litawafanya wawe na ufanisi katika mchakato wa kuendeleza taifa.

(iii) Mabadiliko Maalum ya – Mamlaka ya Jiji la Dar es Salaam

Jiji la Dar es Salaam ni kitovu cha uchumi wa taifa na msingi wa mabadiliko ya jamii kwa jinsi ukusanyaji mapato, ukuaji wa sekta binafsi, uzalishaji ajira, masoko nk. Lakini, utendaji wa jiji unatatizwa na muundo wake wa kiutawala, jambo ambalo linaathiri usimamizi wa mchakato wa maendeleo ya jiji. Kuna mwingiliano wa madaraka ya Manisipaa za wilaya katika Jiji, Manisipaa ya Jiji na Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa ambao unaathiri uratibu wa Mkoa. Matokeo yake ni kwamba, huduma muhimu kama vile Usafirishaji, Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Usimamizi wa Maji na Taka hazijaratibiwa kwa jiji lote. Mpango unapendekeza:

(a) Mabadiliko ya kitaasisi na taratibu za kiutawala za Jiji la Dar es Salaam ili kuboresha uratibu, uwajibikaji, na utoaji/usambazaji huduma. Mabadiliko yanalengo la kuchochea mageuzi ya taratibu ya jiji la Dar es Salaam kuwa Mji Mkuu wa Nchi wenye ufanisi mkubwa kwa kuweka upya wajibu na shughuli za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (DCC) na hasa kuweka wazi madaraka ya kila mdau na kuagiza halmashauri za manisipaa kuratibu huduma kwa Mji Mkuu wote.

(b) Mabadiliko kuruhusu na kufanyia majaribio hatua za kutathmini uwezo wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (DCC) kukusanya mapato yanayolingana na matumizi na kuingiza mifumo inayohakikisha kwamba Halmashauri ya Jiji inawajibika kwa wananchi.

Mabadiliko ya Utawala wa Ardhi

Nafasi na Wajibu wa Mamlaka ya Serikali ya Mitaa.

i. Kuna hitaji la kuwa na kituo kimoja kwa ajili ya masuala ya ardhi ambacho wawekezaji wenye kuhitaji kiwango fulani cha ardhi watakwenda. Hii ina maana kuwa kutakuwa na kituo cha rufaa kwa wawekezaji wanaohitaji ardhi yenye ukubwa ambao uko chini ya mamlaka ya RS na LGAs.

ii. Katika ngazi ya taifa na LGA kuna hitaji la kuwa na benki ya ardhi iliyoundwa maalum kwa maendeleo ya viwanda, yenye huduma za lazima (Hati miliki, skimu ya umwagiliaji maji, barabara ndogo ndogo zinazoingia barabara kuu, nishati, n.k.).

iii. Kuhakikisha hifadhi endelevu la mazingira katika ujenzi wa miji mikubwa na midogo, na majiji, ikiwa ni pamoja na kuimarisha mipango ya maendeleo ya ardhi kwa ngazi ya taifa na ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

SURA 7: UFUATILIAJI NA TATHMINI



Sura hii inaelezea kwa kifupi mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango. Inajumuisha malengo ya jumla na malengo mahsusi, makusudio na viashiria vya kufikia walengwa wa ngazi ya jamii (chini), sekta na mradi au shughuli. Inaeleza taratibu za kitaasisi, wajibu na majukumu pamoja na dhana za mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wenye ufanisi.

Malengo ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E)

Lengo kuu la mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ni kuimarisha majadiliano yenye matunda na wadau. Malengo mahususi ni:

- **Kufuatilia na kuweka kumbukumbu ya maendeleo na kuonyesha matokeo** ya mpango kwa muda mfupi, wa kati na mrefu, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za makusudio ya kimkoa na kimataifa kama vile SDGs ambazo zimeingizwa katika mfumo wa taifa wa maendeleo.
- **Kuratibu na kuwezesha** wizara, idara na wakala za serikali, (MDAs), mamlaka ya serikali za mitaa (LGAs), sekta binafsi, na wadau wengine kufuatilia mara kwa mara na kwa makini maendeleo ya utekelezaji wa vipaumbele vya Mpango.

- ***Tathmini utendaji*** kufuatana na malengo yaliyokubalika na viashiria vya utendaji *na kusudio* ili kusaidia uongozi kupata matokeo (yaani: ufanyaji maamuzi kwa kutegemea uthibitisho), kuendana na sera ya serikali (uwajibikaji) na kujenga mahusiano yenye manufaa na wadau (majadiliano ya kisera na utekelezaji).

- Kuwa na **m*fumo wa utoaji tahadhari mapema*** kwa ***masuala ya changamoto*** au michakato kuhusu utekelezaji wa mpango, ***ambayo inaweza kuhitaji marekebisho ya haraka.***

- ***Kutoa uwanja wa mafunzo endelevu*** kwa ajili ya MDAs, LGAs na wadau wengine wakati wa utekelezaji wa mpango.

- Kuwezesha uandaaji wa ***ajenda za utafiti***, uchambuzi wa kina wa kanzidata (data) katika ukuaji, mageuzi na mwenendo wa maendeleo ya watu, na usambazaji wa matokeo kwa wigo mpana wa wadau.

- Kuendeleza uingizaji na ulinganishaji wa taarifa zinazotokana na ufuatiliaji na tathmini katika uandaaji wa sera, mipango, na uandaaji bajeti katika sekta ya umma hasa pia katika uchumi kwa jumla, pamoja na msaada endelevu wa kiteknolojia na mafunzo kwa ajili ya kuimarisha utamaduni wa M&E kwa ngazi zote nchini Tanzania.

Mkakati wa M&E Utekelezaji wa FYDP II

Mkakati wa M&E wa Mpango una lengo la kujenga mfumo wenye nguvu, wenye upeo mpana, wenye kuunganisha, wenye mpangilio mzuri na unaokubalika, na wenye kuratibiwa vizuri kufuatilia utekelezaji wa shughuli/miradi ya maendeleo ya taifa pamoja na kutathmini matokeo yake ya muda mfupi (outcomes) na ya muda mrefu (impact).

Ofisi ya Taifa ya Takwimu inayo madaraka kisheria ya kutoa mwongozo kwa wizara, idara, na mashirika ya serikali, kuhusu jinsi ya kupata kanzidata kutoka kwenye sekta zao. Kwa MDAs zote, LGAs na mashirika mengine yanayohusika na utekelezaji, mpango wa kati wa miaka mitano utaandaliwa kutafakari juu ya maeneo ya vipaumbele. Mpango utaainisha taratibu za wazi zitakazotumika katika kutengeneza mifumo ya kanzidata, pamoja na kanzidata za kisekta kuanzia ngazi za chini hadi ngazi ya taifa.

Majukumu na Wajibu

Katika kupanga majukumu na wajibu, Mpango unatambua juhudi za awali za kuingiza na kuunganisha shughuli za ufuatiliaji na tathmini katika serikali, ikijumuisha uanzishaji wa vitengo vya M&E katika kurugenzi za sera na mipango katika Wizara zote. Serikali itatakiwa kuanzisha sera ya M&E na sheria yake kama itakavyoonekana kuwa inafaa. Majukumu na wajibu wa taasisi muhimu kama ilivyo katika Mwongozo wa Mpango na Bajeti ni kama ifuatavyo:

Wizara ya Fedha na Mipango:

Wajibu wake ni kuratibu utekelezaji wa Mfumo wa M&E ikiwa ni pamoja na taratibu za ugharamiaji na shughuli mbalimbali zikijumuisha utoaji wa taarifa zifuatazo:

- Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa FYDP II / Taarifa ya Maendeleo (APR).
- Taarifa ya Mageuzi ya Kiuchumi (ETR), hutolewa kila baada ya miaka miwili.
- Umaskini-Taarifa ya Mazingira (P-E Report) kutegemea majaribio ya mbinu za LED na mipango iliyopanuliwa kwa uzoefu huo.
- Taarifa za majadiliano ya kisera yaliyofanyika na utekelezaji wa shughuli/miradi mbalimbali.
- Taarifa za Ufuatiliaji Bajeti na Tathmini yake, kwa ajili ya kufuatilia matumizi ya fedha na uwajibikaji.
- Taarifa za Ujumbe kwa ajili ya ukaguzi wa miradi. (**ujumbe wa timu ya kamati ya bunge katika kukagua miradi**)
- Taarifa za Utendaji wa SDGs.

Ofisi ya Raisi-Usimamizi wa Utumishi wa Umma (PO-PSM):

Ofisi hii inayo wajibu wa kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali watu wanaohitajika kwa uendeshaji wa FYDP II na mkakati wake wa M&E kwa ushirikiano na MoFP kulingana na nguvu kazi (kiidadi na taaluma) inayohitajika kwa uendeshaji wa FYDP II na mkakati wake wa M&E.

Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (MDAs na LGAs):

Watekelezaji wakuu ni wa muhimu kwa utoaji wa taarifa za kila siku na za baada ya kipindi fulani kuhusu maendeleo ya utendaji/utekelezaji kwa kulinganisha na matokeo yaliyopangwa kwa kipindi husika. LGAs watawajibika kutoa taarifa za maendeleo katika utekelezaji na mafanikio ya matokeo ya awali yaliyopangwa (outputs) katika ngazi ya jamii. Hii inahusisha uwekaji msisitizo katika changamoto za kiutekelezaji ikiwa ni pamoja na kufuatilia utekelezaji maalum wa mipango ya maendeleo ya kiuchumi ya jamii (LED) kwa jamii yao.

Washirika wa Maendeleo (DPs):

Washirika wa Maendeleo wanaweza kusaidia mkakati wa M&E kwa kutoa misaada ya fedha na ya kiteknolojia na kusaidia kujenga uwezo kuhusu matumizi ya ufanisi ya taarifa zinazotokana na M&E.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS):

NBS itatoa takwimu na kanzidata ambazo ni muhimu kwa ufuatiliaji na tathmini ya malengo makuu na shughuli za kimkakati za Mpango. Itahusisha upanuzi na utekelezaji wa kina wa Mpango Mkuu wa Kitakwimu uliopo.

Sekta binafsi na washirika wengine wa kimkakati: Sekta binafsi na washirika wengine wasio wa serikali ni wa muhimu katika utekelezaji wa vipaumbele vya mpango; watoaji wa taarifa zinazohitajika katika kupitia sera na taratibu za kiutekelezaji zinazowezesha au kuzuia maendeleo ya biashara na uwekezaji walio na maslahi nao na viwango vya fedha wanayotegemea kuingiza katika huo uwekezaji.

Kwa uwekezaji mkubwa na pale ambapo msaada kutoka sekta ya umma unahitajika, watalazimika kuonyesha mpango kazi wao wa uwekezaji na historia yao katika utekelezaji ili ratiba ya msaada watakaohitaji toka sekta za umma iweze kuandaliwa.

Tathmini ya FYDP II

Kutakuwa na aina tatu zifuatazo za tathmini: Tathmini ya mwaka, tathmini ya muda wa kati na tathmini ya mwisho wa Mpango. Tathmini ya kati na tathmini ya mwisho zitafanywa na mtathmini huru wa kutoka nje ya serikali ili uwazi na ukweli wa hali halisi udhihirike.

Tathmini ya ndani ya mwaka itahusisha uandaaji wa taarifa ya maendeleo ya mwaka (APR), mapitio ya matumizi ya umma (PER) na Mapitio ya sekta ya mwaka ili kuchochea mjadala na taarifa hizo kutumika katika mpango na mchakato wa bajeti. Tathmini ya katikati ya Mpango itafanyika baada ya miaka miwili na nusu itapendekeza mabadiliko yoyote yanayohitajika na kutambulisha "Mkutano wa Mkuu wa nchi wa FYDP II" katika kipindi cha kati cha Mpango kuona kama kuna haja na jinsi ya kurekebisha mwelekeo kama ikibidi.

Tathmini ya Mwisho itafanyika baada ya miaka minne na nusu ambayo itakuwa na sehemu ya taarifa kuu iliyochambuliwa na itatumika katika kupanga jinsi ya kuratibu utekelezaji wa Mpango wa FYDP III utakaoufuata.

MAPENDEKEZO

1) Serikali kuu ipanue wigo wa kodi kwa kuimarisha uwezo wa LGAs kukusanya kodi, kuanzisha mifumo ya kisasa ya usimamizi wa mapato yanayotokana na kodi na wa kukusanya kodi kutoka sekta isiyo rasmi.

2) Serikali kuu idhamirie kuimarisha uhuru wa LGAs katika uamuzi wa vipaumbele vyao vya maendeleo, na katika utafutaji na usimamizi wa rasilimali zao wenyewe.

3) Serikali ihakikishe kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya LGAs zinatumwa kwa kiasi cha kutosha na kwa muda uliopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uendeshaji wa ufanisi wa huduma za jamii.

4) Serikali kwa kushirikiana na wadau husika inatakiwa kuunda utaratibu wa "mwendo kasi" (fast track) ili kuongeza uwezo wa uzalishaji na nafasi za kazi hasa kwa ajili ya vijana na makundi mengine yanayoishi katika mazingira magumu.

5) Serikali kuu itekeleze kwa ufanisi azma yake ya kujenga uwezo wa jamii kupitia ugatuzi wa madaraka ambao unawapa uwezo jamii na LGAs kutumia kwa mbinu endelevu rasilimali zilizoko katika maeneo yao kwa maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi yaliyojumuishi.

6) Serikali itimize ahadi yake kwa wananchi hasa, shilingi za Tanzania milioni 50 kwa kila kijiji na 10% kwa kujenga uwezo wa vijana na wanawake kiuchumi.

Wasiliana nasi:
Kitalu 14, Barabara ya Sembeti, Mikocheni Kwa Warioba,
S.L.P. 38486, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2780200, Simu ya kiganjani: + 255 782 317 434,
Barua pepe: info@policyforum.or.tz, Tovuti: www.policyforum.or.tz